


USALAMA WA NYUMBANI


Kujua kuongoza usalama ya nyumba yako ni kitu kizuri—kwako, kwa benye banaikala na weye, na kwa bajirani yako.

MSINGI WA USALAMA NYUMBANI

Wakati wa kuhamia mu nyumba mupya, kamata wakati wa kufahamu majirani yako na batu ingine benye banaikala karibu yako. Kama unafahamiana na batu mu kikundi yako, itakuwa rahisi kutambua kama kuna kitu chenye haiko sawa ao kama kuna batu benye hauyaonaka



Kwa kukinga usalama wa kila mutu, funga na kufuli milango ya inje kila wakati. Usiruhusu bageni benye hauyue kuingia kwako. Funga na kufuli madirisha kama hauko ku nyumba. Kama uko inje kwa muda mrefu, fikiria kutumia kipima-muda kwa kuwasha na kuzimisha taa ao television kwa automatiki. Bapitanjia banaweza kufikiri kuko mutu mu nyumba. Kufanya hivi itazuia baizi kuingia kwako.



Kwa kumaliza, tumia vifaa vya kunyumba na ku choo kufuatana na maelekezo yake. Kwa mfano, usitumie singa za umeme zenye kuharibika, na ufunge mayi ku lavabo, ku douche, na ku baignoire kama hakuna mutu anaitumia.

USALAMA WA MOTO

Kwa kukinga nyumba yako kwa moto, ujifunze matumizi ya kizimamoto na uelewe namuna kigunduzi ya moshi kinatumikaka. Kama uko mupangayi, mwenye nyumba analazimishwa kuweka kigunduzi ya moshi yenye kutumika pamoja na kizimamoto. *Usitoshe* kamwe batri ya kigunduzi ya moshi. Ukisikia kigunduzi kinalia kwa kifupi na sauti ya juu, badilisha batri.

Hizi ni hatua zingine za usalama wa moto:

- Fanya mpango wa kukimbia moto na familia yako na mujizoeze huyo mpango. Pia, mufanye majaribio ya zimamoto mara kwa mara.
- Usiache moto wenye kuwaka juu ya jiko ao vifaaa vingine vya moto ao vya joto kama hauko karibu. Usitumie kamwe jiko kama vile mashini ya joto wakati wa baridi. Usiweke kitu chochote karibu ya vifaa vya joto nyumbani.



- Usiache kamwe mishumaa ao manukato yenye kuwaka kama hakuna mutu karibu
- Kama una mashini ya kukausha nguo, safisha kichujio mara kwa mara

- Usiache mashini za kufua na kukausha zifanye kazi kama hauko ku nyumba
- Usiache watoto wacheze na vibiriti ao kuviweka karibu yao.



PIGA SIMU 9-1-1

Ni lazima ujue kupiga simu 9-1-1 kuomba msaada kama kuna kitu kinatisha maisha na kinahitaji Polisi, Zimamoto, ao msaada wa kiganga. Mifano ifuatayo inaeleza wakati gani kupiga simu 9-1-1

- Umeshindwa kuzima moto na Zimamoto yako ya nyumbani
- Mutu muovu anajaribu kuingia kwako kwa nguvu ao anatisha familia yako
- Mutu nyumbani kwako anashindwa kupumua, ao anazimia na hawezi kurudishiwa ufahamu, ao alipata ajali mbaya



Ukifuata hii mashauri, utaweza kufanya nafasi ya kuikala yenye usalama na starehe kwako na familia yako.

Cultural Orientation Resource Exchange

For more information, visit Settle In at settlein.us.org.